broadlawns MEDICAL CENTER

# Mpango wa Huduma ya Jamii (CommunityCare) na Msaada wa Kifedha wa Broadlawns Muhtasari wa Lugha Rahisi

### *Ahadi Yetu*

Broadlawns Medical Center hutoa huduma za dharura na huduma muhimu za kimatibabu kwa wagonjwa wote, bila kujali uwezo wao wa kulipa. Pia, tunatoa msaada wa kifedha na punguzo kwa wagonjwa wasio na bima au walio na bima isiyotosheleza ambao wana vigezo vinavyohitajika.

### *Nani Anaweza Kutuma Ombi*

Unaweza kufuzu ikiwa:
- Unaishi katika Kaunti ya Polk na wewe ni raia wa Marekani au mkazi halali.
- Unahitaji huduma ya dharura au huduma nyingine muhimu ya kimatibabu.
- Una kipato au rasilimali chache, au una bili kubwa sana za matibabu ikilinganishwa na kipato chako.

### *Jinsi Punguzo Linavyofanya Kazi*

Punguzo hutolewa kulingana na kipato cha kaya yako ikilinganishwa na Miongozo ya Mapato ya Umaskini ya Serikali ya Shirikisho (Federal Poverty Income Guidelines - FPIG). Ikiwa kipato chako kiko katika kiwango cha au chini ya 600% ya FPIG, unaweza kufuzu kupata msaada wa kifedha wa sehemu au wa gharama zote.

### *Huduma Zinazogharamiwa*

- Huduma za hospitali, kliniki, huduma za haraka (urgent care), na huduma za dharura katika Broadlawns.
- Dawa za kuandikiwa na daktari zinazotolewa na mtoa huduma wa Broadlawns (kiwango maalum)
- Vifaa maalum vya matibabu vinavyotolewa na Broadlawns.
- Miwani ya macho.

### *Huduma Zisizogharamiwa*

- Huduma zinazotolewa nje ya Broadlawns, isipokuwa ziwe zimeidhinishwa.
- Huduma ambazo si muhimu kimatibabu.

### *Jinsi ya Kutuma Ombi*

1. Chukua fomu ya ombi: Inapatikana kutoka kwa Washauri wa Masuala ya Kifedha, wafanyakazi wa kliniki, au kwenye tovuti ya www.broadlawns.org
2. Toa thibitisho la kipato: Risiti za mshahara (pay stubs), fomu za kodi (tax returns), taarifa za Hifadhi ya Jamii (Social Security), au hati nyinginezo.
3. Wasilisha ombi lako: Broadlawns Financial Counseling, 1801 Hickman Rd, Des Moines, IA 50314.
4. Piga simu kwa Mshauri wa Kifedha Aliyeidhinishwa kwa msaada: 515-282-2246.
5. Matokeo: Utapokea uamuzi kwa maandishi. Ombi lako likikataliwa, unaweza kukata rufaa ndani ya siku 10 tangu tarehe ya kukataliwa.

## *Maelezo Muhimu*

- Idhini ya msaada wa kifedha inaweza kudumu kwa hadi miezi 12.
- Ni lazima utoe taarifa kuhusu mabadiliko yoyote ya kipato au bima ndani ya siku kumi za kazi.
- Ikiwa unafuzu kupata bima ya afya, ni lazima utume ombi na kuhakikisha bima hiyo inaendelea kufanya kazi. Hii inaweza kujumuisha Medicare, Medicaid, bima kupitia kazini kwako, au mipango inayotolewa kwenye soko la bima la afya [Welcome to the Health Insurance Marketplace® | HealthCare.gov](https://www.healthcare.gov).
- Wagonjwa walio chini ya umri wa miaka 19 lazima kwanza watume maombi ya mipango ya bima ya jimbo (Medicaid au Hawk-I).
- Msaada huu hutumika tu baada ya vyanzo vingine vyote vya malipo (bima, Medicaid, Medicare) kutumika.

## *Mahali pa Kupata Maelezo Zaidi*

Tembelea: https://www.broadlawns.org/patients-and-visitors/billing-financial
Muulize Mshauri wa Kifedha kwa kupiga simu: 515-282-2246.
Angalia vipeperushi na alama katika hospitali na kliniki zetu.